**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA AFYA**

**BARAZA LA WATAALAM WA MAABARA**
**Tovuti: www.hlpc.go.tz**
**Simu: 0734005777 Barua Pepe:hlpc@afya**

# TANGAZO

**KUFUNGUA DIRISHA LA MAOMBI YA UTARAJALI AWAMU YA PILI NOVEMBA 2024**

Ofisi ya Msajili Baraza la Wataalam wa Maabara inawataarifu wahitimu wote wa Shahada ya Maabara ya Afya ya Binadamu kuwa dirisha la maombi ya utarajali awamu ya pili Novemba litafunguliwa tarehe **25.11.2024** Saa **4:00 Asubuhi** na kufungwa **26.11.2024 Saa 4.00 Asubuhi.** Aidha, Maombi yatafanyika kupitia mfumo wa ***hprs.moh.go.tz***

**Mambo muhimu ya kuzingatia;**

1. Wahitimu wanaoruhusiwa kufanya maombi ya utarajali ni wale walioomba usajili wa awali baada ya kupata barua ya utambulisho kutoka chuoni
2. Wahitimu wote waliosoma nje wanatakiwa kuhakikisha wameambatanisha cheti cha uthibitisho kutoka TCU pamoja na cheti cha matokeo au cheti cha taaluma kutoka chuoni
3. Waombaji wote wanatakiwa wawe wamefanya maombi ya usajili wa awali (Provisional Registration) na awe amepata ujumbe (notification) angalau **yamethibitishwa** (***APPROVED).***
4. Waombaji wote wanasistizwa kufanya maombi kwa wakati na ikitokea mwombaji atahitaji kubadili kituo cha utarajali, anaweza hivyo kuhamia kituo chenye nafasi kupitia akaunti ya mwombaji ya mfumo wa hprs.moh.go.tz kabla dirisha halijafungwa. Baada ya dirisha kufungwa mwombaji wa utarajali **HAKUTAKUWEPO NA UWEZEKANO** wa kubadili kituo cha utarajali.
5. Waombaji ni wahitimu ambao hawakupata fursa ya kufanya maombi awamu ya kwanza. Mhitimu aliyechagua kituo awamu ya kwanza **HARUHUSIWI KUCHAGUA KITUO TENA,** anapaswa kuripoti kituo alichochagua awali.

Aidha, Wote wataopangiwa vituo vya utarajali wanatakiwa kufika Dodoma Ofisi ya Msajili, Baraza la Wataalam wa Maabara tarehe 28.11.2024 Saa 2:00 asubuhi ili kupatiwa maelekezo pamoja na kupatiwa barua.

Ofisi ya Msajili inawatakia waombaji wote utekelezaji mwema

Imetolewa na

Ofisi ya Msajili
Baraza la Wataalam wa Maabara
19.11.2024

HEALTH LABORATORY PRACTITIONERS COUNCIL
19 NOV 2024
P.O.Box 743
DODOMA